

WAKAGURU AU WAKAGULU

Wakaguru ni wabantu. Wakaguru wanapatikana katika mkoa wa Morogoro katika Wilaya ya **Kilosa** na **Gairo**. Sehemu yao ya asili ni sehemu ijulikanayo kama itumba; yaani sehemu za milimani na kandokando ya safu za milima ya Rubeho. Kitovu chao ni kijiji cha **Mamboya**. Hapa kuna pango kubwa la ajabu ambalo lilitumika kujificha wakati wa vita.. Pia kuna Kanisa la Kianglikana ambalo liliua watu mwazoni mwa karne ya kumi na tisa. Kanisa hili lianzishwa zamani sana mwanzoni kabisa mwa ujio wa wamishenari Afrika. Katika misafara yake Dr. Livingstone alipita kijijini hapo na hata baada ya kufa mwili wake ulipita hapo. Misafara ya watumwa ilipita kijijini hapo Mamboya. **Idadi ya Wakaguru kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2006, walikisiwa kuwa 241,000 (2006, Petzell)**

Kutokana na mtawanyiko uliosababishwa na shughuli za Kiuchumi, Wakaguru wameweza kutawanyika na kuingia mikoa mbalimbali ambako wanapatikana kwa wingi. Mikoa hiyo ni Dodoma, Tanga na Manyara. Lugha yao ni (**chikaguru**)

Wakaguru wanaishi maeneo ya **Itumba** wanajulikana kwa jina la **Watumba**. Neno hili linatokana na dhana kwamba watu wanaishi milimani mara nyingi miguu yao huwa imetuna na kufanya misuli. Hii ni kutokana na kupanda na kushuka Milimani. Lakini pia dhana nyingine ni kutana kwa maeneo yao ya asili yaani milima. Lugha yao ina julikana kama **;kikaguru, kigaguru, kiningo, chimegi, kisagara cha kaskazini na kisolwa.**

Taarifa za Wakaguru ziliandikwa miaka ya **1950** na mzungu mmoja aliyejulikana kwa jina la **Beidelman** alipokuwa anatafiti mila na desturi za jamii hii. Alieleza uhusika wa sungura na fisi katika hadithi za wakaguru na wakaguru kuegemea upande wa mama. Hatuna maelezo ya kutosha kuelezea dhana hii.. Beidelman alikaa sana ukaguruni hata aliweza kujifunza kikaguru. Mzungu huyu aliandika mambo mengi sana kuhusu wakaguru lakini kwa bahati mbaya hakuweza kuacha machapisho yake hapa Tanzania. Machapisho yake yaliandikwa kwa lugha ya kingereza na yanapatikana katika maktaba mbalimbali za huko ulaya. Kwa hiyo wakaguru wanajulikana huko ulaya miongoni mwa wasomi wa tamaduni za watu duniani kupitia vitabu alivyoviandika **Beidelman**. Profesa Penina Mlana naye anatupa picha ya jamii hii katika utafiti wake wa shahada ya uzamivu alioufanya kuhusu fasihi ya wakaguru hususani ile inayoambatana na unyago kwa wanawake. Pia yuko mwandishi mwingine Ruth Finegan miaka ya 1960 aliandika kuhusu fasihi simulizi ya Afrika alieza kuhusu wakaguru kuwa ni watu wenye fasihi imara.

Maana ya neno Wakaguru au wakagulu